**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Mkuu wa Shule 0784325395/ 0756079731,**

**Makamu Mkuu wa Shule 0752073186/ 0787722025,**

**Matron/Patron 0688038559/ 0786218010**

**Shule ya Sekondari Emboreet,**

**S.L.P 9596,**

**Orkesumet-Simanjiro.**

**Tarehe .......................**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**……………………………………………**

**YAH: <u>MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI EMBOREET HALMASHAURI YA SIMANJIRO MKOA WA MANYARA MWAKA 2024/25.</u>**

1. Nafurahi kukutaarifu kwamba mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha tano katika shule hii mwaka 2024 na atasoma tahasusi ya CBG/PCB/HGK.

Shule ya sekondari Emboreet iko umbali wa kilometa 90 kusini mashariki mwa jiji la Arusha. Usafiri wa magari kutoka Arusha kuja shuleni Emboreet unapatikana makao mapya stendi inaitwa **MACHAME** na nauli ni shilingi 10,000/=, magari yanaondoka kila siku saa 7:00 mchana.

Ukifika Arusha unaweza kuwasiliana na namba za simu zifuatazo kwa ajili usafiri 0784872216 na 0767872216 (dereva EVANCE MASSAWE) pia namba 0786015974 (dereva HASSAN MKWIZU).

Muhula wa masomo utaanza tarehe 01.07.2024 siku ya mwisho kuripoti ni tarehe 14.07.2024

## 2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.**1 SARE ZA SHULE**

- Mashati mawili meupe yenye mikono mirefu yasio onyesha kwa ndani.(non transeparent),WOTE
- Wavulana suruali mbili(2) rangi Dark Blue yenye marinda mawili,(suruali za mnyonyo zinazobana haziruhusiwi )
- Wasichana sketi mbili (2) rangi ya Dark Blue mshono wa V-Mbele.(ndefu mpaka chini kwenye viunga vya miguu).
- Mabinti wa kiislamu washone suruali ya dark blue badala ya sketi, nusu kanzu nyeupe mshono wa SOLO ya mikono mirefu inayofika magotini isiyo na mpasuo na shungi ndefu nyeupe.
- Sweta rangi Dark Blue mikono mirefu.
- Tai rangi ya Dark Blue pea mbili. WOTE
- Soksi nyeupe pea mbili.
- Viatu pea mbili rangi nyeusi vinavyopigwa rangi nyeusi na kufungwa kamba visiwe na kisigino kirefu.(kwa wasichana baby shoes ZINARUHUSIWA)
- Kwa wavulana, mkanda mweusi usio na bakoli kubwa.

### 2.2 **SARE ZA KUSHINDIA**

**(A) wavulana**

- Suruali mbili rangi ya Maroon (damu ya mzee).
- T-shirt 2 za rangi ya blue.

**(B) wasichana**

- Magauni yenye mshono wa SOLO mawili, Kitambaa cha Drafti ndogondogo za rangi ya blue iliyochanganyika na nyeupe (ndefu mpaka chini kwenye viunga vya miguu).
- Skin tight nyeusi kwa wote na shungi nyeusi kwa mabinti wa kiisilamu.
- Under skirt nyeusi.

## 2.3 SARE ZA MICHEZO

**KWA WOTE**

- Tracksoot pea moja (1) rangi ya BLUE MASAI yenye michirizi myeupe yenye nembo ya shule. zinapatikana shuleni zenye nembo kwa Tsh.30,000/= ( WAWEZA KUNUNUA TRACKSOOT NA KUJA KUGONGEWA MUHURI SHULENI KWA TSH 5,000)
- T-Shirt Nyeupe zenye kola yenye michirizi ya blue (form six). Hizi ni kwa ajili ya kuvalia Tracksoot.
- wavulana bukta moja (1) ya blue.
- wasichana sketi moja fupi rangi ya blue yenye marinda.
- Raba za michezo pea moja (1) rangi NYEUPE.

NB: Sare zote ziandikwe majina.

## 2.4 MAHITAJI MENGINE MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KUJA NAYO SHULENI

**(A). wavulana**

- Mashuka mawili rangi ya light blue.
- Mto wa kulalia na foronya mbili rangi ya light blue

**(B). Wasichana**

- Mashuka mawili rangi ya pinki.
- Mto wa kulalia na foronya mbili rangi ya pink

**NB. Mwanafunzi aje na koti jeusi au sweta zito jeusi lisilo na kofia kwa ajili ya kujikinga na baridi.**

**(C). KWA WOTE**

- Net ya mbu.

- Blanketi moja (1) kuna baridi.
- Mswaki na dawa ya meno.
- Sabuni za kufulia za kutosha
- Sahani, Bakuli, Kijiko, na Kikombe,VYA BATI/ALUMINIUM)
- Sabuni za kuogea za kutosha
- Ndoo mbili(YA PLASTIKI NA YA ALUMINIUM ISIWE YA BATI)
- Jembe na mpini wake.
- Fyekeo.
- Godoro moja futi 2 na nusu kwa 6, yapo magodoro machache shuleni yanakodishwa kwa Tsh. 10,000 kwa mwaka na 5000 kwa muhula.
- Sanduku imara (tranka) kwa ajili ya kuhifadhi vifaa vyake.
- Fagio moja aidha soft bloom,hard bloom,dryer (Kimojawapo)

- Vitabu vya masomo ya tahasusi husika.
- Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biology.
- Mathematical set,kalamu za wino (blue, nyeusi za kumtosha).
- Scientific calculator.
- Madaftari (counter books) ya kutosha 10.
- Kamusi kubwa ya kiingereza (dictionary).
- Begi zuri la kuwekea madaftari.
- Laboratory coat, rangi **NYEUPE**.
- **RIM PAPER** (**A4**) ya karatasi mbili (2) kwa mwaka, moja (1) kwa muhula.

**MUHIMU:** Mwanafunzi aje na bima ya afya asiyekuwa nayo aje na **Tsh. 50400/=** kwa ajili ya kukatiwa bima ya afya.

**2.5 MICHANGO MBALIMBALI**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule **<u>EMBOREET SECONDARY SCHOOL, ACCOUNT NUMBER 42401100019 NMB</u>.** (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay slip. Pay slip iletwe shuleni)

## 3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE NI PAMOJA NA:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;

xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**NB.** Wito wetu ni **NIDHAMU, KAZI NA ELIMU.**

Lengo letu ni kumjenga, mwanafunzi kua na mwendeno mzuri na hivyo kumuwezesha kufanikisha lengo la alichokifuata hapa shuleni. Sheria hizi zitamsaidia kumletea hali ya **AMANI**, **UMOJA** na **FURAHA** awapo hapa shuleni na kumfanya kuwa raia mwema. Kila mwanafunzi aje na nia ya **KUSOMA KWA BIDII** na ajitahidi kuishi vizuri katika jumuiya ya Emboreet Sekondari.

- ***MZAZI ATARUHUSIWA KUWASILIANA NA MWANAE SIKU ZA JUMAMOSI NA JUMAPILI KWA KUPITIA NAMBA ZA MATRONI NA PATRON, MKUU WA SHULE AU MAKAMU MKUU WA SHULE,NA SI VINGINEVYEVYO KAMA HAKUNA DHARURA NYINGINE YEYOTE KATIKATI YA WIKI.***

**VIAMBATANISHO VYA FOMU MUHIMU.**

- Fomu ya Uchunguzi wa Afya (medical examination form) ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa hospitali ya serikali.
- Fomu ya maendelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi, mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.
- Fomu ya mzazi kukiri na kukubaliana na sheria na kanuni za shule, pia kukubali kulipa ada na michango mingine ya shule.
- Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni na namba zao za simu.

  NB: TAFADHARI SOMA MAELEKEZO HAYA NA MAAGIZO KWA UMAKINI ILI UWEZE KUYATEKELEZA KIKAMILIFU.

**KARIBU SANA EMBOREET SEKONDARI**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI EMBOREET
SIMANJIRO

**AZIZA RAJABU MSENGESI**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- ➢ **Mkuu wa shule 0784325395/ 0756079731**
- ➢ **Makamu Mkuu wa Shule 0787722025/ 0752073186**
- ➢ **Mwandamizi Taaluma 0682148678/ 0767528500**
- ➢ **Mwandamizi Malezi 0765180948/ 0687396193**

## SHULE YA SEKONDARI EMBOREET

## FOMU YA KUJIANDIKISHA SHULENI

## HABARI MZAZI/, MLEZI

1. **Jina kamili la baba…………………………………………………………………………**
2. **Kazi yake……………………………………………………………………………………**
3. **Jina kamili la Mama……………………………………………………………………….**
4. **Kazi yake…………………………………………………………………………………..**
5. **Jina kamili la Mlezi (Iwapo mtoto haishi na wazazi wake)………………………………………………………………………………**
6. **Kazi ya Mlezi…………………………………………………………………………..**
7. **Nyumbani kwa Baba(alipo zaliwa mtoto) au place of Domicile**
   **Kijiji/Mtaa………………………….. Wilaya……………………………**
   **Kata………………………………… Mkoa……………………………….**
   **Tarafa……………………………….**
8. **Anwani ya Mahali pa kazi ya baba…………………………………………………..**
9. **Anwani ya mahali pa kazi pa mama………………………………………………..**
10. **Mtoto anaishi na (i)baba tu (ii) mama tuu (iii) wazazi wote (iv)walezi**
    ***kata isiyohusika***
11. **Dini ya baba ………………………….dhehebu……………………………………..**
    **Dini ya mama……………………….. dhehebu……………..……………………**
12. **Anwani kamili ya nyumba ambapo amtoto atakuwa anakwenda siku za zilizo**
    **…………………………………………………………………………………………..**
13. **Namba ya/za simu ya mzazi/mlezi…………………………………………………**
14. **Mimi ………………………….. Baba/mama/mlezi wa……………………………..**
    **Nathibitisha kuwa taarifa hiyo hapo juu ni sahihi na nina a**
    **hidi kushirikiana na walimu ili kuhakikisha kwamba kijana wangu anakua na tabia nzuri, mchapa kazi na mwenye bidii ya masoma.**

**Tarehe………………………………….**

**………………………..**
**Sahihi ya mzazi/ mlezi**

# FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA UTII

**Mimi ………………………………………….. (jina kamili) kidato cha ……………**

**Mwaka ………………nakubali na nina ahidi kufuata taratibu za shule kama zilivyopangwa nikienda kinyume nichukuliwe hatua za kinidhamu.**

**Tarehe…………………………….** **…………………………………….**
**Sahihi ya mwanafunzi**

**Tarehe……………………………..** **………………………………………**
**Sahihi ya Shahidi**

**Tarehe…………………………….** **………………………………………**
**Sahihi ya Mkuu wa Shule**

**PRESIDENT'S OFFICE, REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT.**
**EMBOREET SECONDARY SCHOOL.**

To be completed by Medical Government Hospital in a respect of all-new entrants of Emboreet Secondary school,

Full Name……………………………………………………………….

Age……………………………………………………………………

i. Skin……………………………………………………………
ii. Blood count (red and white)……………………………………
iii. Urine Examination…………………………………………….
iv. Stool examination…………………………………………….
v. Syphilis Test ………………………………………………..
vi. T.B Test…………………………………………………….
vii. Ear Test……………………………………………………
viii. Eye Test ………………………………………………..
ix. Spleen ……………………………………………….
x. Abdomen …………………………………………..
xi. Additional information of any other physical mental hereditary of infection

………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………..

Treatment after Examination

……………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………

(Please state nature of treatment)

**MEDICAL CERTIFECATE:**

I certify that the above mentioned has been examined and found fit to pursue further education.

Signature…………………………………

Designation……………………………….

Station……………………………………..

Date ……………………………………….. Official Stamp……………………….

## ORODHA YA VITABU MUHIMU UNAVYOPASWA KUWA NAVYO KAMA UNAWEZA KUJINUNULIA.

### <u>A-LEVEL CHEMISTRY</u>

- ESSENTIAL OF PHYSICAL CHEMISTRY (By S.CHAND)
- INORGANINIC CHEMISTRY PART A&B
- CONCEPTUAL CHEMISTRY VOL I(xi) and VOL II (xi)----By CHAND
- NGAIZA PHYSICAL CHEMISTRY

**A-LEVEL BIOLOGY**

- BIOLOGICAL SCIENCE By TAYLOR,3rd Edition
- UNDERISTANDING BIOLOGY By GLENN and SUSAN TOOLE
-
- ADVANCE BIOLOGY By MICHAEL KENT

**A-LEVEL GEOGRAPHY**

- GENERAL GEOGRAPHY IN DIAGRAM By R.B BUNNET
- RESEARCH METHODOLOGY By KOTHARI CR
- MAN AND ECONOMIC GEOGRAPHY By MSABILA DT(For Geo. II)
-

**A-LEVER PHYSICS**

- PRINCIPLES OF PHYSICS FOR ADVANCED LEVEL BY NELKON & PARKERS.
- PRINCIPLES OF PHYSICS FOR CLASSF xi BY CHAND
- PRINCIPLES OF PHYSICS FOR CLASS xii BY S.CHAND
- UNDERSTANDING PHYSICS BY ROGER MUNICASTER

**A-LEVEL GENERAL STUDIES**

- UNDERSTANDING ADVANCED LEVEL GENERAL STUDY
- ADVANCED LEVEL SECONDSRY SCHOOL EDUCATION by Joannes and Sospeter M. Deogratias
- GENERAL STUDIES PAPER REVIEWS any of resent year.

**A-LEVEL KISWAHILI**

**KISWAHILI (01)**

1. Shule za sekondari – Kilangi Enock Lucas
2. Taasisi ya Elimu Tanzania – (**TIE**) (**V-VI**)
3. Nadharia ya Lugha Kiswahili Sarufu (**SAMAKISA**) sekondari na vyuo-Kihore (**Y.M**)
4. Kamusi ya Kiswahili sanifu, Toleo la pili, Masamba,
   (**D.P.B, TUKI (2023)3 – ENGLISH-SWAHILI DICTIONARY LAZIMA.**

**KISWAHILI (02)**

1. Fasihi kwa Ujumla- Kilangi Enock Lucas (**V-VI**)
2. Nadhana ya Fasihi kidato cha Tano na sita-Msebo (Oxford University Press
3. Tahakiki ya vitabu teule vya Fasihi (Kilangi Enock Lucas) kidato cha (**V-VI**) **LAZIMA**
4. **TIE** (Taasisi ya Elimu Tanzania- Kiswahili (02) shule za sekondari

## A- LEVEL HISTORY

**HISTORY I**

1. Essential in Advanced Level History paper 1
2. Advanced History for secondary schools student's book form five (**TIE**)

**HISTORY II**

1. Essential in advanced level History paper 2
2. Advanced History for secondary school student's Book form six. **(TIE**)